

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Simu Nambari: 2152532/3  
Baruapepe: [cg@dcea.go.tz](mailto:cg@dcea.go.tz)  
Tovuti: [www.dcea.go.tz](http://www.dcea.go.tz)  
Nukushi: 2152820



8Barabara ya kivukoni,  
S.L.P. 80327,  
Dar es Salaam.

### TAARIFA KWA UMMA

#### UTEKETEZAJI WA KILO 250.7 ZA DAWA ZA KULEVYA

##### **Mtwara, 22 Februari 2022:**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, leo tarehe 22 Februari, mwaka 2022 imeteketeza jumla ya Kilo **250.7** za dawa za kulevya zinazojumuisha kilo **51.7** za heroin na kilo **199** zenye mchanganyiko wa heroin na cocaine katika kiwanda cha saruji cha Dangote mkoani Mtwara.

Uteketezaji huo ni kwa ajili ya kutekeleza amri ya Mahakama iliyotolewa katika kesi Namba 2 ya Mwaka 2018 kwenye kikao cha Mahakama Kuu kilichoketi mkoani Lindi mbele ya Jaji Latifa Mansour mwishoni mwa mwezi Oktoba na kumalizika tarehe 5 Novemba 2021. Kesi hiyo iliwahusisha washtakiwa Sano Sidiki na Tukure Ally ambao wamehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 20 gerezani kila mmoja.

Amri nyingine ya uteketezaji ilitolewa na Mheshimiwa Jaji Isaya Arufan tarehe 29 Novemba, 2021 kwenye kesi Namba 25 ya mwaka 2019 iliyowahusisha washtakiwa Mohamed Nyamvi na Ahmad Said Mohamed. Katika kesi hiyo washtakiwa hao walihukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 20 kila mmoja.

Zoezi hili limefanyika kwa mujibu wa Kanuni Namba 14 ya Kanuni za Kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya za mwaka 2016 za Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Namba 5 ya mwaka 2015. Kanuni hiyo inaelekeza kuteketeza dawa za kulevya baada ya shauri kumalizika Mahakamani na kwa dawa za kulevya zenye tabia ya kubadilika au kuharibika endapo zitakaa kwa muda mrefu uteketezaji wake unaweza kufanyika kabla au wakati Shauri husika linaendelea kusikilizwa Mahakamani.

Uteketezaji huu ni wa pili kufanyika katika kiwanda cha saruji cha Dangote kwani tarehe 15 mwezi Juni mwaka 2021, ulifanyika uteketezaji mwingine uliojumuishwa jumla ya **kilo 355** za dawa za kulevya aina ya Methamphetamine. Zoezi la uteketezaji limekuwa likifanyika katika viwanda vya Saruji kwa lengo la kuepuka dawa hizo kuharibu mazingira na kuathiri afya za watu.

Uteketezaji wa dawa za kulevya umefanyika kwa uwazi mbele ya wadau wote muhimu wanaotambulika Kisheria na kushuhudiwa na Waandishi wa Habari ili kuondoa dhana iliyojengeka kwa baadhi ya wananchi kwamba, baada ya dawa za kulevya kukamatwa hurejeshwa mtaani na kuuzwa tena.

Mamlaka inatoa shukrani kwa wadau wote walioshiriki katika kufanikisha zoezi hili muhimu la uteketezaji. Kipekee inamshukuru mwekezaji wa kiwanda cha saruji cha Dangote kwa kuendelea kutupatia ushirikiano kwa kuruhusu zoezi hili kufanyika kiwandani hapa. Pia, Mamlaka inawasihi wananchi kuendelea kutoa taarifa juu ya watu wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya ili kwa pamoja tuweze kuishinda vita hii na hatimaye kuifikia Tanzania yenye kizazi kisichojihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Imetolewa na,



Daniel Kasokola

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
**Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**